



EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

MAOMBI YA TAARIFA YA KUONYESHA NIA YA KUTOA HUDUMA YA TEHAMA PAMOJA NA VIFAA VYA TEHAMA KUMBUKUMBU NA. 10007040

TotalEnergies East Africa Midstream B.V. (Kampuni) Tanzania, kampuni ya kimataifa ya nishati, inaalka makampuni/taasisi yenye sifa na uzoefu katika kutoa huduma pamoja na vifaa vya teknolojia ya Habari na mawasiliano katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha Mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta hayo katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni karibia kilomita 1,443, kati hizo kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania. Uendelezaji wa Mradi wa EACOP unahusisha uandisi wa kina, ujenzi, uendeshaji na uboreshaji wa miundombinu ya Mradi.

MAELEZO MAFUPI YA MAWANDA YA HUDUMA:

Ili kutekeleza majukumu yake, Kampuni inahitaji huduma kutoka kwa wakandarasi wenye uzoefu na sifa nzuri katika kutoa huduma za miundombinu ya mawasiliano pamoja na huduma za mfumo wa kompyuta ikiwemo utatuzi wa changamoto. Huduma zinazotarajiwa ni:

- Utoaji wa huduma za vifaa: kompyuta na mfumo wake, simu na vifaa vinavyoambatanana na matumizi ya simu, kufunga mfumo wa umeme na mawasiliano (cabling), mtandao, mfumo wa kuhifadhi taarifa (server) na vifaa vinavyohusiana na huduma hizi.
- Mafunzo kwa timu ya watendaji na watumiaji.

- Huduma za ziada za ushauri (kama vile uundaji, usimamizi wa mfumo, pamoja na ukaguzi).
- Huduma za mawasiliano ya simu.
- Huduma za usaidizi katika uendeshaji pamoja na marekebisho.

Kama ilivyo katika matakwa ya Kampuni katika vipengele hivi:

- Kipengele cha kwanza: miundombinu ya mtandao uliojikita kwenye mfumo wa Cisco.
- Kipengele cha pili: mfumo wa uhifadhi taarifa (server) uliojikita kwenye mfumo wa Microsoft Azure na NetApp.
- Kipengele cha tatu: Mfumo wa kompyuta binafsi uliojikita kwenye mfumo wa Windows, Android na simu za iOS, Microsoft Office 365 na Azure.
- Kipengele cha nne: Mfumo wa usalama mtandaoni.
- Kipengele cha 5: Huduma za kuchapisha.
- Kipengele cha 6: huduma za mawasiliano ya simu.
- Kipengele cha 7: Mfumo wa moja kwa moja (fixed) wa kupata huduma za mtandao.

VIGEZO MUHIMU:

- Uwezo wa kifedha wa kutekeleza mkataba.
- Uthibitisho wa uzoefu wa kutoa huduma tajwa.
- Uzingatiji wa Kanuni za Maudhui ya Wazawa za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Wazawa (Nafasi za Ajira na Huduma kwa Watanzania).
- Usajili katika Kanzi Data ya Watoa Huduma wa Ndani ya EWURA (LSSP) katika kipindi cha kuwasilisha nia kwa ombi hili yanahimizwa.
- Mkandarasi LAZIMA awe na cheti cha ushirika cha watendaji/watoa huduma katika soko.

Makampuni yenye nia, uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliziwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: eacop-tz.eoi.100001@totalenergies.com (ukubwa usiozidi MB20) kichwa cha habari kikiwa ni kumbukumbu namba husika hadi kutikia saa 11:00 jioni Majira ya Afrika Mashariki, tarehe 27 Sept. 2021 Makampuni yaliyokidhi vigezo muhimu pekee ndiyo yatakayopata fursa ya kuwekwa kwenye orodha ya makampuni ya awali yenye vigezo.